JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TANO

KIKAO CHA TISA

06 NOVEMBA, 2026

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TANO

KIKAO CHA TISA – TAREHE 06 NOVEMBA, 2026

I. DUA:

II. KIAPO CHA UAMINIFU NA AHADI YA UZALENDO KWA WABUNGE:

Mhe. Dkt. Netho Ndijina Ndilito

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

123. MHESHIMIWA EMMANUELA KAGANDA MTATIFIKOLO (ISIMANI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Malenga Makali.

124. MHESHIMIWA GEORGE NATANY MALIMA (MPWAPWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Soko la kisasa katika Mji wa Mpwapwa ambao kwa sasa hauna Soko.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

125. MHESHIMIWA JUMA OTHMAN HIJA (TUMBATU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaelimisha Wananchi Hoja zote za Muungano zilizokwisha kupatiwa ufumbuzi ili wazielewe.

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

126. MHESHIMIWA NAJMA MURTAZA GIGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, kwa nini Serikali haitungi Sera ya Taifa ya malezi kwa Watoto na Vijana ili kukabiliana na kuporomoka kwa maadili.

WIZARA YA NISHATI:

127. MHESHIMIWA MARY FRANCIS MASANJA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Wananchi wa Vijijini wanaoathirika na matumizi ya nishati chafu watafikiwa ili kuendana na Agenda ya kumtua Mama kuni kichwani.

IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

(i) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2026 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments (No.3) Bill, 2026];*

(ii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa Mwaka 2026 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments (No.4) Bill, 2026];*

(iii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Madini wa Mwaka 2026 *[The Mining (Amendment) Bill, 2026];*

(iv) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira wa Mwaka 2026 *[The Environmental Management (Amendment) Bill, 2026];*

(v) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Sekta ya Famasi wa Mwaka 2026 [*The Pharmacy Sector Laws (Amendment) Bill, 2026];* na

(vi) Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Usafiri Majini Tanzania wa Mwaka 2026.

V. TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE:

VI. HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE:

WAZIRI MKUU:

VII. WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA AFRIKA MASHARIKI:

DODOMA **BARAKA I. LEONARD**
06 NOVEMBA, 2026 **KATIBU WA BUNGE**